GRACE COMMUNION INTERNATIONAL

Living and Sharing the Gospel

MUONGOZO WA KUHUBIRI/KUFUNDISHA

NEEMA NA UTII

Na Gary Deddo

Translated to Kiswahili by:
Francis Nyoike
Nairobi Kenya Congregation
nyoikefg@gmail.com

NEEMA NA UTII

Imeandikwa na Gary Deddo na inapatikana katika tofuti ya www.gci.org

Kufuatia karne za mjadala, ni dhahili wakristo hawajapata ufafanuzi mwafaka kati ya neema (imani ya Mungu katika neema ndani ya Yesu Kristo) na utii (Kutii sheria). Wahuburi ambao misingi yao imetokana na mafunzo mazuri ya Biblia wanajua hakika kuwa ukombozi ni kazi ya Mungu na unapatikana kwa imani. Wanatambua vile vile kuwa maisha yanayotokana na imani katika Kristo yanahusu utii. Shida inatokea unapojiuliza ni jinsi gani utafuata moja bila kuadhiri (au bila kupuuza) nyingine. Changamoto ni kuepuka kutotii au kutafuta utakatifu kupitia kwa matendo.

UJUMLA WA, NA?

Wengi wanatambua uhalali wa neema na utii (imani na matendo). Badala ya kufuata njia panda ya ama, au, wengi wanakumbatia mtazamo wa ujumla wa, na.(yaani kuzingatia imani na vile vile matendo mema) Japo mtazamo huu unayomachache kuhusu “na” na kuhusu jinsi gani neema na utii zimeunganishwa. Matokeo yake ni kuwa neema na utii kiubinadamu zimeunganishwa pamoja au zimepangwa pamoja moja juu ya nyingine. Ni kama kwamba zimewekwa kwenye chumba kimoja na kuamrishwa zipatane. Kufuatia mtazamo huu juhudi za kufanya marekebisho kwenye mitazamo potovu katika upande (neema) mmoja zinamaanisha kusisitiza upande (utii) mwingine.

Kwa hali hiyo, dini nyingi zinasisitiza moja au nyingine, ikitegemea ni ipi wanayofikilia huenda ni hatari au inavutia. Huwa Napata kuwa matokeo ya mitazamo ni kama ule mchezo wa kuinuana mtu

mmoja anakaa upande mmoja na mwingine upande wa pili na wanainuana kwa kutegemea ni yupi mwenye uzani zaidi (seesaw), ambapo mshikamano kati ya sheria (matendo) na neema (imani) haieleweki au haipo kabisa.

Katika hali tofauti, huwa Napata Biblia inaoanisha na kuhusianisha neema na utii kama mambo ya msingi katika imani ya Mkristo na maisha yake.

Kwa mfano, katika kitabu cha Warumi 1:5 na 16:26 mtume Paulo anasema kuleta uoanisho huu ndio lengo la msingi la injili yake.

Katika Warumi 14:23 anasema utii wowote usiotokana na imani katika neema ni dhambi! Waraka kwa Wahebrania 11 anatoa mifano ya watu waliomtii Mungu “kwa imani”. Pia katika waraka wa kwanza wa Yohana 5, tunaambiwa kuwa amri za Mungu sio nzito kwetu kwa sababu ya hiyo imani yetu (fungu la 3-4).

Yesu mwenyewe katika Mathayo 11:29-30 anatukumbusha kuwa Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi. Yesu pia anatukumbusha sisi ni marafiki wa Mungu sio watumwa (tazama Yohana 15:15) halafu katika waraka kwa Wagalatia Paulo, anatwambia “Imani inafanywa imara kupitia kwa upendo” (Wagalatia 5:6)

HALI INAYOUNGANISHA NEEMA (IMANI) NA UTII (MATENDO) - "NA"

Yapo mafungu chungu nzima katika agano jipya yanayofafanua uhusiano kati ya Neema (imani) NA utii (kumpenda Mungu na wanandamu). Lakini kiunganishi hiki kinafanya kazi vipi? Je kiunganishi hiki kikoje? Kiunganishi hiki kinapatika ndani ya Yesu Kristo ambaye peke yake na ndani yake anadhihirisha tabia, akili, mtazamo na mpango wa Mungu.

Tunachoshikilia katika imani yetu ni Yesu Kristo na nia na makusudi yetu ni kumwamini Yesu kuwa ni Mungu kutokana na yeye ni nani na yale aliyoyatenda kwa niamba yetu. Basi kwa hali hiyo imani ni mwitikio wetu kwa kumtambua Yesu mwenyewe, maneno yake na pia matendo yake. Tunaweka imani yetu kwa Mungu kwa kuzingatia Yesu Kristo ni nani. Na yeye mwenyewe ndiye neema ya Mungu kwetu.

Yesu Kristo ndiye injili. Ndiye wokovu. Na tunapokea manufaa yote ya uhusiano wetu naye tunapoweka imani yetu kwake na kuweka kando (kutumbu) vitu vinavyo pinga imani. Kufuatia hayo tunashiriki uhusiano wa dhati na mshikamano na Yesu kama mwokozi na Mungu wetu. Maisha yetu yanaunganishwa kwake na tunashiriki katika maisha yake, tukishiriki naye katika yale yote anayoyafanya, tukiyafanya katika uhusiano wetu wa imani.

Tunapata uzima wetu katika uhusianoo na mshikamano na Yesu Kristo, tukipokea kutoka kwake yale yote aliyonayo naye akipokea yale yote tunayomkabidhi. Katika uhusiano na mshikamano huo tunabadilishwa, hatua kwa hatua (2 Wakorintho 3:18 Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile

katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho). Ili kushiriki zaidi ndani ya Yesu aliyeinuliwa, tabia na mienendo yake, tunatakiwa kujikita ndani ya kazi ya neema kupitia kwa Roho Mtakatifu pamoja na kwamba mengi hayajafunuliwa kwetu na bado tumesalia kuwa wanadamu katika ulimwengu (2Wakorintho 4:7)

MTAZAMO WETU KWA YESU:
Tatizo lililopo ni kuwa wanadamu wanaomtazamo finyu sana kwa Yesu na hili linadhoofisha imani yetu. Pamoja na kwamba wanamwamini kwa wokovu wa baadaye (Kuingia Binguni), imani yao inaishia hapo. Licha ya hayo, tunapotazama maandiko kwa kina zaidi, tunaona kwamba Yesu ni mwokozi na vile vile ni Jemendali. Yesu anatuokoa kwa neema na vile vile anaamrishi mambo kwetu.

Tunatambua dhahiri kuwa utii wetu hautununulii wokovu, basi kwa nini utii ni wa muhimu? Labda tunafikilia tunatakiwa kutii kwa kuwa Jemendali wetu ameamrishi hivyo- kwa kuwa ni mkuu, anayo nguvu na ni vema tutii vinginevyo….. kwa mtazamo huu basi, utii unakuwa ni kujitoa kwa amri tunazofikilia labda tunalazimishwa na Mungu ambaye maamuzi yake hayabadilishwi, basi huu unakuwa utii wa Utumwa!

Tatizo kuu la utii wa namna hii inaonyesha mtazamo mfinyu sana ya uelewa wa Yesu na anachotupatia. Tunatakiwa kuelewa ujumla wa Yesu, yeye ni nani na jumla ya yale anayotoa kwetu ili tupate kushika kinachotufanya tumuamini. Tunatakiwa kuanza kwa kuelewa kuwa Yesu ni Bwana wa yote, ulimwengu mzima na Bwana wa mambo yote. Pili tuelewe kuwa anaompango na nia njema kwa

ulimwengu wote. Analeta ukombozi kwa vitu vyote na kufanya upya ulimwengu na hata mbingu. Yeye ndiye Bwana na mwokozi juu ya kila sehemu ya maisha yetu na analo kusudi la kila nyanja ya uwepo wetu. Anakusudia tuwe mfereji wa Baraka zake kwetu na kupitia kwetu kwa wengine wote. Kwa haya yote, kila uhusiano unalenga kuelekeza watu kwa maisha bora ya uhusiano na Kristo.

Hata mambo mandogo kama kula, kunywa inatakiwa kudhihirisha upendo wa Mungu anayetupatia maisha (1 Korintho 10:31).

Uhusiano wetu na watu wote unatakiwa kudhihirika kama zawadi ya matunda mema yanayotokana na mchango wa maisha kamilifu ya upendo wa Yesu. Mmlaka ya Yesu yanagusa kila sehemu ya maisha, kila sehemu ya uwepo na mtazamo wetu, iwe hesabu, fisikia, utafiti wa madawa, biolojia, wanyama, maisha ya kawaida, mahusiano, lugha, tamaduni, sheria, uchumi, mawazo na fikra zetu, dini na hata ibada zetu. Na haya yote chimbuko lake ni uhusiano wetu na Mungu kupitia kwa Yesu Kristo.

Uhusiano huu kati yetu na Mungu kupitia kwa Yesu Kristo unapenya kila sehemu ya maisha yetu chini ya mamlaka ya ukombozi wa Yesu. Neema ya Mungu inahusika katika mambo haya yote. Huu ndio msingi wa mitazamo ya ulimwengu. Kwa hali hiyo kila tunalolipokea kutoka kwa Mungu tunawapatia wanadamu wenzetu ili kueneze upendo na nia ya Mungu katika ulimwengu.

Hii inapaswa kudhihirika hasa katika mahusiano yetu. Tumepokea msamaha wa dhambi – kufanywa upya katika neema ili tuanze maisha upya katika tumaini. Tunapokea fadhili za Mungu anapotukabidhi uwezo wa kupata matunda ya Roho Mtakatifu.

Tunapokea faraja, upendo, nguvu za kubadilishwa na maana na mwelekeo wa maisha ili tuwe kama ishara na ushuhuda wa neema na wema wa Mungu.

Tunakuwa mashahidi wa ukweli na tabia ya upendo ya Mungu. Na mambo haya yote yanatuelekeza kwa maisha ya milele – maisha pamoja na Mungu sisi tukiwa kama wanawe, katika mshikamano wa upendo.

AMINI NA UTII.

Imani yetu kwa Mungu kupitia kwa Yesu katika mambo haya yote, sio tu kwa nia ya "kwenda Binguni" wakati mmoja. Kila amri ya Mungu na kila utii umeshikanishwa na vipengele vya sababu ya kumtii Mungu. Tunasamehe kwa sababu tumesamehewa kwanza, tunapenda kwa kuwa Mungu alitupenda kwanza. Tunapenda adui zetu kwa kuwa Mungu alitupenda kwanza (na anakusudi njema) kwa adui zake na zetu pia.

Tunaweza kuwa wakarimu kwa kuwa Mungu ni mkarimu kwetu. Tunaweza kuwa wakweli kwa kuwa Mungu ni mkweli, mwaminifu na ataufunua ukweli nyakati za mwisho. Tunaweza kuwa wabunifu na wa msaada kwa kuwa Mungu ni mbunifu na ni wa msaada kwetu. Tunawafariji wengine wakati wa huzuni kwa kuwa Mungu anatufariji wakati wa huzuni.

Tunavumilia wengine kwa kuwa Mungu ni mvumilifu kwetu. Tunakuwa wapatanishi kwa kuwa Mungu ni mpatanishi. Tunatafuta haki na uhusiano mwema katika hatua zote za maisha kwa kuwa Mungu ni mwenye haki na mtakatifu. Tunaunganisha kwa kuwa Mungu ni muunganishi. Matendo yetu yote ya imani ni kushiriki

kwa yale Mungu anayoyafanya kupitia kwa Yesu Kristo na Roho Mtakatifu. Hii ina maana kuwa wote tuko kwenye ushirika na tumeungana na Kristo. Hatujajitenga kwa kuwa tumeunganishwa na Kristo kama ndugu na dada katika familia ya Mungu.

MAMBO YA MSINGI YANAYODHIHIRIKA KUTOKA KWA MAELEZO HAYA.

Tunatii kwa imani tunapotambua ushirika wa Kristo katika kila tukio, mwamini kuwa ni mwaminifu katika tukio husika na utende kwa kuamini kuwa kweli ni mwaminifu. Kwa kifupi, tunatenda kwa imani ndani yake tunayemwamini. Utagundua kuwa, kila amri katika mafungu ya Biblia huwa ikielekeza tabia mojawapo ya Mungu na yale unaweza kumwaminia.

Tunapotambua uhusiano kati ya yale Mungu anaweza kuaminiwa kutenda, na yale anayotuelekeza kutenda basi hali hii inazalisha kutii kwa imani. Mwana thiolojia James Torrance aliongelea haya kwa kusema kuwa kila jambo la msingi la imani limejengwa katika msingi uliosimikwa katika neema.

Kiini cha uhusiano huu ni kwa sababu amri zote Mungu anazotupatia (maelekezo yote ya msingi) yanatokana na tabia yake, moyo, mtazamo na kusudi lake hata yale yote ametutendea ndani ya Yesu Kristo (yanayodhihirika). Mungu hatendi kwa kiburi – wapenzi yake kwetu kila wakati yanaongozwa na kudhibitiwa na tabia na nia yake katika ushirika wa nafsi tatu za Uungu, ambaye alikuja kwetu ndani ya Kristo ili tupate ushirika na unganiko naye katika upendo mtakatifu.

Kwa hali hiyo, neema ya Mungu inatokana na imani ndani ya Mungu kwa sababu ya Yesu Kristo na utii kwa Mungu wa neema inatokana na imani kwa Mungu kwa sababu ya Yesu Kristo. Kwa hali hiyo imani na utii zinachimbuka kutoka sehemu moja – imani ya Mungu katika Yesu. Zote mbili ni kujitoa kwetu kwa kutambua Yesu ni nani kwetu. Zote mbili zinamisingi yake katika thiolojia ya ushirika wa nafsi tatu za Uungu, kufanyika kwa mwana wa Mungu kuwa Binadamu. Zote mbili ni matokeo ya uhusiano wa kumwamini Mungu kupitia kwa Yesu Kristo ndani ya Roho.

MWONGOZO WA KUHUBIRI/KUFUNDISHA.

Ifuatayo ni miongozo ambayo nimeiandaa ili kusaidia kuweka neema na utii pamoja ndani ya Kristo:

a. Katika kuhubiri/kufundisha usije ukaagiza washiriki kutii kabla hujawaonyesha jambo ambalo uaminifu wa Mungu utadhihirika katika wanalotakiwa kutii. Tafuta jambo la msingi la neema litakalo tokana na jambo wanalotakiwa kutii katika mafungu ya Biblia.

b. Katika mafunzo/mahubiri kila wakati fafanua tabia ya neema, wokovu, urejesho wa Jemedali. Usije akamuonyesha Mungu kama Jemedali ambaye ni mkatili ambaye Roho yake, mawazo yake, mienendo na nia yake imejitenga na tabia, mienendo tunayoiona ndani ya Kristo. Kila mara anza kwa kujibu maswali ya msingi, “U nani wewe Bwana?” kwa kufanya hivyo mahubiri/mafundisho yetu yanakuwa kweli yanafafanua nafsi tatu za Uungu na Mungu kufanyika binadamu.

c. Katika mafunzo/mahubiri, usiwahi kufuata mapenzi au uchaguzi wa mwanadamu. Katika analochagua mwanadamu, kuna msukumo wa ubinadamu, tumaini, upendo, hisia za uoga, imani au kutoamini. Kwa kifupi, katika kila tendo kuna kuamini au kutoamini Mungu. Jitahidi sana kuhubiria mioyo ya washirika, msukumo wa Roho ndani yao, wito wao wa kubandili tabia, nia na mapenzi ya Mungu kwa ushirika wao na Mungu. Fafanua yale Mungu anaweza kushirikishwa kwa, kuaminiwa kwa, lisha imani zao, wape matumaini na upendo wa Mungu. Utii utatililika kutokana na mafunzo haya.

d. Usihubiri "Kama ……..Basi Mungu" mahubiri ya aina hii, hupelekea watu kufuata sheria kwa hofu na matendo yasiyo ya imani mbali ya kufuata sheria. Badala ya hiyo hubiri/fundisha hivi "Kwa kuwa Mungu ndani ya Krsito…… basi wewe……" au "Unapofanya X, Y au Z, kutokana na imani…… utapokea yale Mungu anatoa ndani ya Kristo."kwa mfano sema "Tunapotumbu dhambi zetu tunapokea msamaha ambao Mungu tayari ametupatia ndani ya Kristo."

e. Dhihirisha utii kama "kwenda kufanya kazi pamoja na Mungu" kama tendo la ushirika na Mungu ambalo Roho wa Mungu anatuhusisha ndani ya analotenda Mungu.

f. Hubiri utii kama "kiunganishi kati ya" lakini sio "Lazima U." Hubiri utii kama upendeleo wetu kama wana wa Mungu, sio kama kitu cha kung'ang'ania au unaotuleta kwenye utumwa kwa Mungu.

g. Usiuonyeshe utii kama hitaji la kuunganisha pengo kati la Mungu mtakatifu na wanadamu walionguka kutokana na tendo la dhambi. Sio wito wetu kujenga ufalme au kuifanya nia ya Mungu idhihirike. Lakini fundisha uhalisi wa Mungu na anayoyatenda (aliyoyatenda), eleza wito wetu kushiriki pamoja na Mungu kudhihirisha uhalisia huo. Kwa mtazamo huu, lililobaki kwetu ni kudhibitisha na kushiriki katika ukweli ambao Mungu ameudhibitisha ndani ya Kristo kupitia kwa Roho au kupuuza na kukataa kushiriki. Hatuna nguvu za kubadili ukweli huu bali kuchagua kama tutaupokea na kushiriki.

h. Hubiri na ufundishe neema ya Mungu kama tendo lililokamilika – ukweli kuwa ndio tegemeo letu hata kama kwa sasa imefichika. Usiifundishe kama tukio litakalo tokea kama tutafanya X, Y, au Z. Mungu hategemei matendo yetu. Bali, ametualika tushiriki ndani ya yale ameshayatenda, anayoyatenda na atakayoyatenda. Hubiri kama alivyohubiri Kristo: “Ufalme wa Mungu uko nasi, tumbuni dhambi zenu na muamini katika habari njema.” Hubiri kama Petro: “Kwa kuwa Mungu amemfanya Yesu Bwana na Mwokozi, basi tumbuni na muamini.” Tambua lengo au nia ya ujumbe huu imewakilishwa kama kutakiwa kwetu kujitoa kutokana na ambayo Mungu ni nani, na kutokana na yale tayari ametenda.

i. Usihubiri kama kwamba Mungu hawezi kuwa mwaminifu kuliko tulivyo sisi. Kama kwamba tunamzuia Mungu kutenda anayokusudia kutokana na matendo tunayoyafanya au tusiyoyafanya. Paulo anasema kwamba: “Kama sisi hatuamini, yeye hudumu wa kuaminiwa. Kwa maana hawezi kujikana

mwenyewe." (2 Timotheo 2:13). Tunaweza tusishiriki kama inavyotakiwa kushiriki, lakini Mungu atatekeleza malengo yake mazuri. Mungu hatuhitaji, lakini anafurahi kushirikisha wanawe katika anayoyatenda. Tuliumbwa ili tushiriki (mshikamano na ushirikiano) pamoja na Mungu.

j. Usiwape wanadamu uwezo wa kuleta uhalisia. Kama kwamba tunayoyatende "ndiyo tu yanayoleta madabiliko yanayotakiwa". Kristo peke yake ndiye anayepokea sifa. Matendo yetu, yawe makubwa au mandogo (hata kama ni kikombe cha maji au imani yetu ni kama mbegu ya haladali), inatoshana na mikate michache na samaki kulisha watu elfu tano. Sio kubwa kama au ndogo kuliko, hii ikituelekeza itakavyo kuwa katika ufalme wa Mungu. Sisi ni mashahidi tu, na matendo yetu ya kuudhihirisha ni sehemu tu, yenye upungufu, yasiyodumu na ya muda tu. Lakini kwa neema ya Mungu, maandiko yanatumia mambo haya mandogo kutuelekeza kwa Kristo ili imani yetu iwe kamilifu kwa kuzingatia yeye ni nani.

k. Tambua kwamba utatakiwa kuamini bila shaka kuhusu neema ya Mungu isiyo na masharti ili kuleta utii wa imani ili kuweza kuhubiri na kufundisha kwa njia hii na kuepuka kusawishika kurudi kwenye imani ya kuonekana kama neema ya Mungu inategemea ukumbali wetu. (na hivyo kutegemea matendo yetu).

l. Tambua kwamba wewe kama Paulo, hutaweza kuwazuia wengine kutenda maovu wakijificha ndani ya mafunzo ya neema (japo kujificha huku hakutawafanya waipokee, lakini

watakuwa wameikataa). Wakati mwingine utalaumiwa na wengine kama Paulo, alivyo laumiwa kwamba anawasihi washiriki kutenda dhambi na kutotii. Lakini Paulo hakubadili ujumbe wake hata baada ya wao kulaumu. Tusijaribu kuzuia kukataliwa au watu kujificha katika neema kwa kubadili ujumbe wetu tukaanza kufundisha utii wa utumwa kama ilivyofanyika Galatia. Kufanya badiliko hilo itakuwa kuisaliti injili ya Mungu ndani ya Yesu Kristo.

Ni matumaini yangu kuwa maelezo haya ya Biblia yameweza kuleta pamoja Neema na Utii kwa mpangilio, kibinafsi na njia iliyooanishwa vizuri ili pasiwe na “ama, au” au kuichukulia kiurahisi kama “zote, na.” Wanaompenda na kumwamini Mungu kupitia kwa Yesu Kristo, ndani ya Roho kama Bwana wa ulimwengu watatamani kuwa waaminifu kwake na kuwa naye katika kila mtazamo katika maisha haya na sasa, hata katika hali ya upotovu tuliyo nao duniani.

Nukuu:

Nukuu: